

Anwani ya Simu: "ELIMU" Simu: 026
296 35 33
Barua pepe: info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz



Mji wa Serikali - Mtumba,
Mtaa wa Afya,
S.L.P 10,
40479 DODOMA

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. CA.229/238/01/21

1 Desemba, 2022

Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais – TAMISEMI,
Mji wa Serikali - Mtumba,
Mtaa wa TAMISEMI,
S.L.P 1923
41185 DODOMA.

MWONGOZO WA KALENDA YA MIHULA KWA SHULE ZA AWALI, MSINGI NA SEKONDARI KWA MWAKA WA MASOMO WA 2023


Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu.

2. Kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na idadi sahihi ya siku za masomo ili kutekeleza Mtaala kwa ufanisi, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeandaa **Kalenda ya Mihula ya Masomo kwa Shule za Awali, Msingi na Sekondari kwa Mwaka wa Masomo wa 2023**. Kalenda hii inatakiwa ifuatwe na kuzingatiwa ipasavyo ili kupata matokeo chanya.
3. Hivyo, Kalenda ya Mihula ya Masomo kwa Shule za Awali, Msingi na Sekondari kwa Mwaka wa Masomo wa 2023 itakuwa kama ifuatavyo:

MIHULA	KUFUNGUA MUHULA	LIKIZO FUPI		KUFUNGA MUHULA	IDADI YA SIKU ZA MASOMO
		KUFUNGA	KUFUNGUA		
Muhula I	09/01/2023	31/03/2023	11/04/2023	31/05/2023	94
Muhula II	03/07/2023	01/09/2023	18/09/2023	07/12/2023	100
Jumla ya Siku za Masomo					194

Tanbihi:

- Siku za Masomo kwa mwaka ni 194.
 - Mashindano ya UMITASHUMTA yatafanyika tarehe 02/06/2023 hadi 13/06/2023, na UMISSETA yatafanyika tarehe 15/06/2023 hadi 26/06/2023.
 - Mashindano ya Michezo ya Shule za Sekondari za Afrika Mashariki (FEASSSA) yatafanyika kuanzia tarehe 18/08/2023 hadi 28/08/2023.
4. Mwongozo huu utanza kutumika tarehe 01 Januari, 2023.
 5. Nawatakia utekelezaji mwema.



Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
KAMISHNA WA ELIMU

Nakala:

Katibu Mtendaji,
Baraza la Mitihani Tanzania,
S.L.P 32019,
DAR ES SALAAM.

Wathibiti Wakuu Ubora wa Shule Kanda na Wilaya,
TANZANIA BARA.